

DAWASA YETU

TAREHE: 14 SEPTEMBER - 21 SEPTEMBER 2024 | TOLEO NA. 0175

KAMATI YA BUNGE YAVUTIWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA BILIONI 200 DAR



Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira imeipongeza Serikali ya **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kufanya **uwekezaji mkubwa** kwenye utekelezaji wa miradi ya kisasa ya takribani **Bilioni 200** katika uboreshaji wa **Usafi wa Mazingira Dar es Salaam na Pwani**.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Maji na Mazingira Mhe. Jackson Kiswagwa (Mb) amesema kuwa **kamati** imetembelea na kukagua **utekelezaji wa mradi** wa ujenzi wa mitambo ya kisasa ya kuchakata takatope katika **Wilaya ya Kinondoni na Ubungo** ambayo inauwezo wa kuchakata **lita 780,000** za majitaka kwa siku. Pamoja ma **mradi wa kuchakata majitaka** wa **Mbezi Beach** unaolenga **kunufaisha wakazi 11,488** wa **Kata ya Mbezi Beach, Kawe, Wazo na Kunduchi**.



Ameeleza kuwa baada ya kutembelea utekelezaji wa miradi hii Kamati imeridhishwa na mipango iliyopo ya **Mamlaka** ya kuondosha majitaka kutoka majumbani ambapo kiasi cha uchafu kinachozalishwa **Dar es Salaam** kinachakatwa na kurejeshwa na **kuzalisha maji ghafi** yatakayotumika kutunza **mazingira** pamoja na gesi itakayotumika kama **nishati mbadala**.

Kwa upande wake Waziri wa Maji **Mhe. Jumaa Aweso** ameipongeza **Serikali** kupitia **DAWASA** kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika miradi ya kuboresha Usafi wa Mazingira **Dar es Salaam na Pwani**, pamoja na kufanya ziara ya kukagua uwekezaji kwenye **miradi ya majitaka**. Hii ni mojawapo ya huduma muhimu kwa wateja baada ya kuboresha **huduma ya majisafi**. Hatua hii inachagiza jitihadaa za kuhakikisha ifikapo **mwaka 2030** tuwe na uwekezaji wa **kiwango cha asilimia 30** katika **Usafi wa Mazingira**.

DAWASA MOJA, NGUVU MOJA, KAZI IENDELEE